JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS - TAMISEMI
HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOSHI
SHULE YA SEKONDARI MSARANGA

Mkurugenzi:
SIMU: 2752344
S.L.P 318
MOSHI

Shule ya Sekondari Msaranga
S. L. P 1902
Moshi
Tarehe

Kumb. Na.MRS/MMC/MSS/J/021

Ndugu,

YAH. MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MSARANGA.

1. UTANGULIZI.

Nina furaha kukujulisha kwamba umechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza Shule ya Sekondari Msaraanga mwaka 2021.
Shule hii ni ya kutwa na mchanganyiko, na iko kando kando ya barabara kuu ya kwenda Dar Es Salaam. Shule ipo umbali wa Km4.5 kutoka mji wa Moshi. Wewe ni miongoni mwa wanafunzi wachache waliobahatika kuendelea na masomo, hivyo unatakiwa kuwajibika kikamilifu katika kutekeleza maagizo yote kwa utii, busara, hekima, utii na uaminifu.
Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe **11 / 01 / 2021**, mwanao anatakiwa kuripoti shuleni asubuhi **saa 1 : 30 asubuhi bila kukosa.**

2.0 Mambo ya kuzingatia

2.1 Sare za shule

(a) Sare ya shule ni kitambaa cha rangi ya **"dark blue".** Zingatia mashono yaliyoelekezwa: Zenye **rinda box** na urefu ufikie chini ya magoti. Kwa wote, shati nyeupe za mikono mifupi pamoja na sweta za rangi ya dark blue. Kwa wanaovaa hijabu, iwe nyeupe sawa na shati l a shule, bila kuwa na urembo wowote.
(b) viatu vya rangi nyeusi vya kufunga na gidamu na visiwe na visigino kirefu
(c) Soksi kwa wote ni nyeupe zisizo na mapambo
(d) Kwa wavulana, mkanda wa ngozi, rangi nyeusi na usio na bakoni kubwa
(e) Daftari 11 (**angalau quire 3**), mkebe wa mahesabu, kalamu, mkebe wa mahesabu (Mathematical Set) pamoja na begi imara la kuhifadhia vifaa hivi.

3.0 Sheria na kanuni muhimu za shule hii.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheriaa ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978. Na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo:

(a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima;
(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima;
(c) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa;
(d) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
(e) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
(f) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapokuwa shuleni;
(g) Kungatia ratiba ya shule wakati wote;
(h) Kushiriki kwa bidii ya hali ya juu katika kujifunza unapokuwa darasani; na nje ya darasa kulingana na ratiba ya masomo;
(i) Kutunza mali za umma

4.0 Makosa yafuatayo yanaweza kusaababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule:

(a) Wizi

(b) Uasherati na ushoga

(c) Ubakaji

(d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli, na kadhalika.

(e) Kupigana au kupiga

(f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma

(g) Kudharau Bendera ya Taifa

(h) Kuwa mjamzito/kupata mimba

(i) Kuoa au kuolewa

(j) Kutoa mimba

(k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.

(l) Kukataa adhabu kwa makusudi.

(m) Kuwa na simu ya mkononi.

5.0 Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi:

(a) "Medical Examination form" ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakaporipoti shuleni.

(b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo, na makosa ya jinai.

(c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

(d) Nakala ya cheti cha kuzaliwa.

Tafadhali soma kwa makini maelekezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII.

_____

MKUU WA SHULE

OFISI YA RAIS – TAMISEMI
HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOSHI
SHULE YA SEKONDARI MSARANGA
FOMU YA TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI YA KUKUBALI SHERIA NA NAFASI YA SHULE ALIYOPEWA.

A. TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI

JINA LA MWANAFUNZI (LA MTIHANI WA DARASA LA SABA)
……..
TAREHE YA KUZALIWA (AMBATANISHA NAKALA YA CHETI CHA KUZALIWA)
…….
MAHALI ALIPOZALIWA; WILAYA…….. MKOA……
……
…
URAIA: MTANZANIA / SI MTANZANIA ……..……..
SHULE YA MSINGI ALIPOHITIMU DARASA LA SABA……..
NAMBA YA MTIHANI WA TAIFA ALIYOITUMIA KUFANYA MTIHANI WA DARASA LA SABA ……

B. TAARIFA YA MZAZI/MLEZI:
JINA LA MZAZI…….…
ANWANII YA MZAZI/MLEZI……..
KUKUBALI NAFASI NA MAELEZO ALIYOPEWA MWANANGU:

Mimi …….ninakubaliana na nafasi aliyopewa mwanangu, na ninaahidi kuwa nitatoa ushirikiano wa kutosha.

Saini …….Tarehe……

C: MWANAFUNZI KUKUBALI KUFUATA SHERIA NA MASHARTI YA SHULE:

Mimi ……..nimezisoma na kuzielewa sheria za shule na ninaahidi kwamba nitakuwa ninatii sheria zote na maelekezo yote nitakayopewa na walimu na viongozi wote wa shule.

TAREHE ……SAINI .....

D: TAARIFA ZA SERIKALI ZA MITAA ANAKOTOKEA MWANAFUNZI.

MTAA ……. KATA ……. WILAYA ……
JINA MWENYEKITI WA KITONGOJI / MTAA
……
NAMBA YA SIMU …… SAINI NA MHURI…..……..

PRESIDENT OFFICE
REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
KIBORILONI SECONDARY SCHOOL BOX. 441, MOSHI. PHONE 0763318438
REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

To be completed by Medical Officer from a recognized Governmental Hospital.
……..
……..
Full Name of the Student
……..……
Sex: ……..

Please examine the student named above who has been selected to join this school for his / her fitness as a student in the following areas:
1. Eye sight ……

2. Hearing …… …….

3. Specimen
   (i) Stool …….
   (ii) Urine …… …….
   (iii) Blood …… …….

4. Asthma / Tuberculosis …….. …….
5. Pregnancy …… ……
6. Other diseases …….. ……
   - …… ……
   - …… …….
   - …….. ……
   - ……

MEDICAL CERTIFICATE
(To be completed by the medical Officer)
I have examined the above and considered that he / she is physically fit as a student.

Date…… Signature……. ……..

Station …… Designation …….

OFFICIAL STAMP